**TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB.) KWA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU UTEKELEZAJI WA AHADI YA SERIKALI YA KUAJIRI WATUMISHI WAPYA 44,096, KUPANDISHA VYEO WATUMISHI 92,619 NA KUBADILISHA KADA WATUMISHI 6,026 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo hapa leo hii tukiwa na afya njema. Kipekee naomba kuwashukuru na kutambua mchango wenu Waandishi wa Habari katika kuwafikishia Watanzania taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya kiutumishi na utawala bora.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa nia, jitihada na maono yake makubwa ya kuboresha Utumishi wa Umma nchini

kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo tuliyonayo.

Tangu kuingia kwake madarakani, Mhe. Rais ameweza kutoa dira na maelekezo yenye lengo la kuboresha Utumishi wa Umma ili kuimarisha maadili, nidhamu uzalendo, uwajibikaji pamoja na kusimamia haki na stahiki za Watumishi wa Umma na Watendaji mbalimbali Serikalini ili kuongeza tija, moyo wa kufanya kazi kwa bidii na uwajibikaji wa hiari kwenye Utumishi wa Umma.

Nia njema ya Mhe. Rais katika eneo la uboreshaji wa maslahi ya watumishi inajidhihirisha kupitia uamuzi wake wa kutoa idhini ya kuajiri watumishi wapya, kupandisha vyeo watumishi pamoja na kubadilisha kada.

Mhe. Rais amekuwa akifanya haya yote ili kuziwezesha taasisi za umma kuwa na rasilimaliwatu ya kutosha yenye ujuzi na maarifa stahiki katika kuufanya Utumishi wa Umma kuwa na tija na hatimaye kusaidia utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kusaidia katika maendeleo ya nchi na

ujenzi wa uchumi wa nchi yetu. Tunamuombea Baraka kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema na maisha marefu.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kama mnavyofahamu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kisera la kusimamia uendelezaji sera katika Utumishi wa Umma, Utawala wa Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Mishahara, Usimamizi wa Mifumo ya Uendeshaji wa Serikali, Usimamizi wa Mifumo ya Utendaji Kazi wa kila Siku Serikalini, Uendelezaji Rasilimaliwatu, Ukuzaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma, Usimamizi wa Serikali Mtandao na Usimamizi wa Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma.

Katika kutekeleza jukumu la Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Mishahara, Ofisi hii ina dhamana ya kusimamia ajira za watumishi wa umma na mgawanyo na mtawanyo wake ndani ya Utumishi wa Umma, udhibiti wa Ikama na Bajeti ya mishahara, upandishaji vyeo pamoja na ubadilishaji wa kada kwa watumishi wa umma.

***Ndugu Waandishi wa Habari***

Pamoja na masuala mengine nitakayoyazungumza, lengo kuu lililotukutanisha mahali hapa leo ni kuwafahamisha kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuajiri watumishi wapya **44,096**, kupandisha vyeo watumishi **92,619** na kubadilisha kada watumishi **6,026** kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kama mtakavyokumbuka katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali iliidhinishiwa nafasi **44,096** za ajira mpya, nafasi **92,619** za kupandisha vyeo watumishi pamoja na kuwabadilishia kada/vyeo (Re-categorization) watumishi **6,026** kwa kada mbalimbali. Kati ya nafasi **44,096** za Ajira mpya, Serikali kupitia Taasisi zinazotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (Human Capital Management Information System-HCMIS) imeshaajiri

watumishi **12,336** wakiwemo watumishi **11,492** wa ajira mpya na watumishi **844** wa ajira mbadala hadi sasa. Watumishi hawa wanaendelea kutekeleza majukumu yao katika taasisi mbalimbali za umma.

**A: AJIRA MPYA**

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kama itakavyokumbukwa kupitia taarifa yangu kwa vyombo vya habari wakati wa Uzinduzi wa Mfumo wa Kielekroniki wa Tathmini ya Hali ya Watumishi katika Utumishi wa Umma nilibainisha kwamba mahitaji ya watumishi kwa taasisi za Umma yapo kati ya asilimia 52 hadi 90. Kwa kutambua hilo na katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi pamoja na maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha fedha zinapatikana na ajira zilizo bajetiwa kwa mwaka wa fedha 2021/22 zinatolewa, Serikali imeamua kutekeleza ahadi yake ya kuajiri watumishi wengine **32,604** kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha na mchakato wa ajira hizi unaanza leo.

Niseme tu Taarifa hii ni hatua ya kwanza ya mchakato wa kuhakikisha utekelezaji wa ajira hizo unakamilika kabla ya mwaka wa fedha 2021/22 haujaisha. Utekelezaji wa Ajira hizi utaigharimu Serikali kiasi cha shilingi **26,297,541,175.00** kwa mwezi sawa na Shilingi **315, 570,494,100.00** kwa mwaka.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kwa kutambua juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha Taifa linapata maendeleo ya haraka ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya ujenzi wa uchumi na inayotoa huduma iliyoasisiwa na Serikali zilizopita na ile iliyoanzishwa na inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Miradi ya UVIKO 19, Serikali imetoa kipaumbele katika Sekta za Elimu, Afya.

Pamoja na Sekta hizo, Serikali imezingatia mgawanyo wa ajira katika Sekta nyingine zikiwemo Kilimo, Maji, Mifugo, Uvuvi pamoja na maeneo mengine yenye uhitaji wa watumishi kwa mchanganuo ufuatao:-.

1. **Sekta ya Kipaumbele ya Elimu** imetengewa jumla ya nafasi **12,035** zikiwemo:-

   (i) Nafasi 9,800 kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

   (ii) Nafasi 2, 235 kwa ajili ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu pamoja Wakufunzi wa Vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Taasisi husika za elimu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

2. **Sekta ya Kipaumbele ya Afya imekasimiwa nafasi za ajira 10,285** zinazojumuisha:-

    (i) Nafasi 7,612 kwa ajili ya Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

    (ii) Nafasi 1650 kwa ajili ya kuajiri watumishi wa kada za Afya katika Hospitali za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa; Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Wizara ya Afya; na

    (iii) Nafasi 1023 kwa ajili ya Vyuo vya Afya, Hospitali nyingine za kimkakati na zile za Mashirika ya Dini (District Designated Hospitals-DDHs) na Hiari ( Voluntary Agency-VAHs) zenye mkataba na Serikali. Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Wizara ya Afya kwa Vyuo vya Afya na Hospitali nyingine za kimkakati na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kwa Hospitali za DDHs na VAHs.

**3.** Nafasi **2,392** zinatarajiwa kujazwa kwenye Sekta zingine za kipaumbele ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kada za Kilimo nafasi za ajira 814. ;

(ii) Kada za Mifugo nafasi 700;

(iii) Kada za Uvuvi nafasi 204;

(iv) Kada za Maji nafasi 261; na

(v) Kada za Sheria nafasi 513.

Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Wizara pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

**4.** Nafasi **7,792** kwa ajili ya kuajiri Watumishi wa kada nyingine kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma.

Mchakato wa ajira hizi utasimamiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

## B: UPANDISHAJI VYEO NA UBADILISHAJI WA KADA

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kwa kutambua umuhimu wa rasilimaliwatu na kwa lengo la kuboresha maslahi ya watumishi, Serikali pia itawapandisha vyeo/madaraja watumishi **92,619 na** Serikali itatumia jumla ya Shilingi **23,078,224,169.50** kwa mwezi sawa na Shilingi **276, 938,690,034.00** kwa mwaka na kuwabadilisha vyeo/kada (Recategorization) watumishi **6,026** waliotengewa Ikama na Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuanzia tarehe 01 Mei, 2022. kwa gharama ya Shilingi **824, 441,522.00** kwa mwezi sawa na Shilingi **9,893,298,264.00** kwa mwaka.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kwa mantiki hiyo na kwa kutambua kwamba hivi karibuni Serikali iliwapandisha vyeo/madaraja Watumishi **190,781** wenye sifa stahiki katika kipindi cha mwaka mmoja wa utawala wa Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jumla

ya watumishi wa umma **282,400** watakuwa wamepandishwa vyeo katika kipindi hiki kifupi. Aidha, jumla ya watumishi **25,412** watakuwa wamebadilishiwa kada katika kipindi tajwa.

Haya ni mafanikio makubwa na inadhihirisha nia thabiti ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kushughulikia haki na stahiki za Watumishi wa Umma.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Maamuzi haya ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwapandisha vyeo na kuwabadilisha kada watumishi wa Umma yataongeza ari, motisha na uwajibikaji wa hiari kwa watumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Nichukue fursa hii kuwataarifu kwamba kwa mara ya kwanza, upandishaji vyeo kwa watumishi **92,619** utafanywa moja kwa moja na Mfumo wa Mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) kwa kutumia Orodha ya Watumishi wenye sifa (Eligibility List) iliyopo kwenye Mfumo huo.

Waajiri watawajibika kuandaa na kuwapa barua za kupanda cheo baada ya watumishi hao kupokea mishahara mipya inayoendana na cheo/daraja jipya kwa ajili ya kumbukumbu za kiutumishi.

Uidhinishaji huu utawezesha watumishi wote **92,619** kupata mishahara ya vyeo vipya kwa wakati moja, hivyo kuondoa ucheleweshaji katika upandishaji wa vyeo pamoja na uzalishaji wa malimbikizo ya mishahara. Nitumie fursa hii kuwakumbusha waajiri kupitia tena Orodha ya Watumishi wenye sifa (Eligibility List) iliyopo kwenye Mfumo wa HCMIS kwa lengo la kujiridhisha iwapo watumishi husika bado wana sifa na vigezo vya kupandishwa vyeo hadi sasa.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Naomba kutumia nafasi hii kuziagiza Mamlaka za Ajira, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Afya pamoja na Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kuhakikisha wanaendesha michakato ya ajira hizi kwa uwazi, weledi, uadilifu pamoja na kutoa fursa sawa kwa waombaji wote kuweza kushiriki katika mchakato huu na hatimaye Serikali

iweze kupata watumishi mahiri na wenye sifa stahiki. Napenda pia kuwaasa baadhi ya waajiri kutotumia fursa hii kuajiri watumishi wazembe au wasiotekeleza majukumu yao kikamilifu kwa lengo la kujaza nafasi kwani jambo hili halikubaliki na halitavumiliwa kwa namna yeyote. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itafuatilia mchakato mzima wa ajira hizi hatua kwa hatua ili kuhakikisha Serikali inapata watumishji wenye sifa na ubora ambao wapo tayari kulitumika Taifa.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kwa upande wa upandishaji vyeo na ubadilishaji kada, nawakumbusha waajiri wote kuhakikisha zoezi tajwa linafanyika kwa haki na kwa wakati kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa katika Miundo ya Utumishi ya kila kada pamoja na mambo yote yaliyoainishwa katika Kanuni D.51 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009 ikiwa ni pamoja na Tange (Seniority List) iliyohuishwa na kuwepo kwa nafasi iliyoidhinishwa katika Ikama.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Pamoja na maelekezo haya, nichukue fursa hii kuagiza mambo yafuatayo:-

a. Waajiri wote kuhakikisha wanawapangia majukumu stahiki watumishi wapya wote na kusimamia ipasavyo rasilimaliwatu iliyopo kwenye maeneo yao ya kazi ili kuleta tija kwa maendeleo ya taifa. Tukisimamia ipasavyo rasilimaliwatu, rasilimali nyingine zote tulizonazo zitaweza kutumika ipasavyo katika kutuletea maendeleo katika sekta mbalimbali hapa nchini.

b. Taasisi na Mashirika ya Umma yote nchini ambayo hayajaingizwa katika Mfumo Mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na yanalipa mishahara kwa kutumia fedha zitokanazo na mapato ya ndani zikamilishe maandalizi muhimu ya kuingia na kuanza kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (New HCMIS) **kabla au ifikapo tarehe 30 Juni, 2022**.

c. Maafisa wenye dhamana ya kusimamia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) wahakikishe wanachukua hatua madhubuti katika kudhibiti Watumishi na Mishahara Hewa ikiwa ni pamoja na kusitisha katika Mfumo ajira za watumishi wanapokoma kuwa watumishi wa umma kwa sababu mbalimbali zikiwemo kustaafu, kuacha kazi kufukuzwa kazi, kufariki, likizo bila malipo, kugombea nafasi za kisiasa na kumalizika kwa mikataba ya ajira. Waajiri na Maafisa watakaobainika kusababisha kuwepo kwa watumishi na mishahara hewa watachukuliwa hatua kali za kinidhamu/kisheria kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

d. Waajiri wote wakamilishe zoezi la kusafisha taarifa za kiutumishi na mshahara ili kuondoa mianya ya kuwepo kwa watumishi na mishahara hewa kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll). Pamoja na faida nyingine, hatua hii itauwezesha Mfumo wa HCMIS kuwaondoa moja kwa moja (automatically) kwenye

"Payroll" watumishi pindi utumishi wao unapokuwa umekoma kwa sababu ya umri.

e. Ofisi hii kwa kushirikiana na Waajiri ikamilishe zoezi la Tathmini ya Hali ya Watumishi katika Utumishi wa Umma kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Tathmini ya Hali ya Raslimaliwatu katika Taasisi za UMama kama ilivyopangwa ili kuiwezesha Serikali kuwa na taarifa sahihi ya hali halisi ya Watumishi na hatimaye kuwa na msawazisho stahiki wa watumishi wa Umma katika taasisi zote za umma.

f. Waajiri wote nchini wahakikishe watumishi wa umma wapya wote watakaoajiriwa wanapata mafunzo elekezi (Induction Course) kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma kabla ya kupangiwa vituo vya kazi kama ilivyoelekezwa na Serikali.

g. Watumishi watakaoajiriwa wanaagizwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, maarifa na kwa ubunifu pamoja na kuwajibika kwa hiari bila shuruti kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Nichukue fursa hii kuwaasa waajiri na waombaji wa ajira mpya kujiepusha na vitendo vya rushwa na udanganyifu hususan wa vyeti vya elimu na taaluma wakati  na baada ya mchakato wa ajira hizi. Nitumie fursa hii kuiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) kufuatilia kwa karibu mchakato mzima wa ajira hizi ili kuweza kubaini na hatimaye kuzuia mianya yote ya rushwa na upendeleo.

**Ndugu Waandishi wa Habari**

Kwa niaba ya Ofisi yangu niwashukuru tena kwa ushirikiano wenu ambao mmekuwa mkiutoa pindi tunapowahitaji, na niwahakikishie kuwa Ofisi yangu itaendelea kufanya kazi nanyi bega kwa bega katika masuala ya kiutumishi ambayo wananchi wana haki ya kuhabarishwa.

***KAZI IENDELEE***

**Ninawashukuru kwa kunisikiliza**